# MIFUMO YETU

**Jarida la Mifumo ya TEHAMA ya TAMISEMI**

TOLEO NA. 12 Februari 2020 — Aprili 2020



MFUMO WA UKUSANYAJI WA MAPATO
YA MAMLAKA
ZA SERIKALI ZA MITAA
LGRCIS
Mapato kwa Maendeleo
Tumeboresha mapato
na kuinua maendeleo
TAMISEMI ya wananchi

*Jarida hili limeandaliwa kwa ushirikiano kati ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3).*

*" Jarida hili limefanikishwa kwa msaada wa watu wa Marekani kupitia Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID), chini ya Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3). Ofisi ya Rais -TAMISEMI ndiyo itakayowajibika na matokeo ya kazi hii. Jarida hili ni maoni ya*

*Ofisi ya Rais-TAMISEMI, na si lazima liwakilishe maoni ya USAID au Serikali ya Marekani"*

USAID
KUTOKA KWA WATU WA MAREKANI

**USAID/TANZANIA UIMARISHAJI WA MIFUMO YA SEKTA ZA UMMA**

UHURU NA UMOJA

# Bodi ya Uhariri


## Mwenyekiti
*Mhandisi. Joseph M. Nyamhanga*
*Katibu Mkuu – Ofisi ya Rais, TAMISEMI*

## Wajumbe
*Erick Kitali – TAMISEMI*
*Desderi Wengaa – PS3*

## Waandishi
*Atley Kuni - TAMISEMI*
*Stella Kalinga – Kondoa Mji*
*Hyasinta Kissima – Njombe Mji*
*Tusa Daniel– Tanga Jiji*

## Mhariri Mkuu
*Gladys Mkuchu– PS3*

## Wahariri
*Erick Kitali – TAMISEMI*
*Desderi Wengaa – PS3*
*Atley Kuni - TAMISEMI*
*Enock J. Mmari-TAMISEMI*
*Gladys Mkuchu – PS3*

## Msanifu Kurasa
*Jacqueline Sombe – PS3*



## Jarida hili hutolewa na:
*Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa-TAMISEMI*
*(Mji wa Serikali Mtumba)*
*S.L.P 1923*
*Dodoma-Tanzania*
*Simu: (+255) 26 -2321234*
*Barua pepe: ps@tamisemi.go.tz*
*Tovuti: www.tamisemi.go.tz*
*Blogu: blog.tamisemi.go.tz*
*Facebook: Ofisi ya Rais – TAMISEMI*
*Instagram: ortamisemi*

## Ndani ya Jarida Hili:

**Tahariri………………………………………………………………………………………........uk 6**

**Wananchi na Watendaji Wasifu Ubora wa Mfumo wa LGRCIS…...…...………….……….…...uk 7**

**LGRCIS yapatiwa Mashine za Kisasa Kudhibiti Mianya Upotevu Mapato….……....…......uk 8**

**LGRCIS Yasaidia Halmashauri ya Mji Njombe Kuongeza Bajeti Kufikia Bilioni 4………..uk 10**

**LGRCIS Mkombozi wa Makusanyo ya Mapato Kondoa……………………………….........uk 12**

***TAHARIRI:***

# Mfumo Thabiti wa Ukusanyaji Mapato

Historia ya mfumo wa kukusanya mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa inajengwa katika mlolongo wa miaka zaidi ya nane iliyopita. Uwepo wa mfumo thabiti kwa sasa ni maboresho ambayo mfumo umepitia kuanzia mwaka 2012 na ni ishara ya maendeleo katika ukusanyaji wa mapato kwa kutumia mfumo huu ambao unafahamika kwa lugha ya Kiingereza *"Local Government Revenue Collection Information System- LGRCIS"*

Ofisi ya Rais-TAMISEMI tangu mwaka 2012 ilipoanza matumizi ya mfumo huu, imefanikiwa kuzifikia Mamalaka za Serikali za Mitaa zote185 nchini. Mfumo umeleta manufaa katika mchakato wa ukusanyaji na usimamizi wa mapato, uwazi na uwajibikaji.

Kujizatiti huku kwa Ofisi ya Rais,TAMISEMI katika mifumo kunaenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia yanayotokea duniani kote. Kama taifa hatuwezi kukaa nyuma wakati wenzetu wanakimbia, hivyo lazima tutambue kuwa matumizi ya mifumo ni agenda muhimu sana katika kusukuma mbele gurudumu la maendeleo.

Kwa kutambua hilo, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, imefanikiwa kuunganisha mfumo huu na mfumo wa Serikali uitwao GePG , zaidi sana imeongeza mashine mpya na za kisasa za kukusanyia mapatao *"Point Of Sale - POS-Mchine"* zipatazo 7,227. Ugawaji wa mashine 7,227 za POS na kufanya idadi katika Mamalaka za Serikali za Mitaa kufikia 17,327 Mashine zote hizi zinakwenda kuongeza nguvu ya uwezo wa kukusanya mapato.

Katika toleo hili la 12 la Jarida la Mifumo Yetu, msomaji wetu ataweza kujisomea makala kadhaa ambazo zimeandikwa na wataalam wetu kutoka ngazi ya Halmashauri kuelezea kwa kina jinsi ambavyo mfumo huu ulivyo rafiki na wenye tija katika kufanikisha ukusanyaji na usimamizi wa mapato, uwazi na uwajibikaji.

Nawatakiwa usomaji mwema wa Jarida hili la Mifumo Yetu Toleo la 12 na kwa pamoja tuendeleze gurudumu la maendeleo katika ukusanyaji wa mapato kwa maendeleo ya nchi yetu.

Asanteni

**Mhandisi Joseph M. Nyamhanga**

**Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais -TAMISEMI**

*KUTOKA TANGA JIJI*

# Wananchi na Watendaji Wasifu Ubora wa Mfumo wa LGRCIS

Wananchi na Watendaji wa Jiji la Tanga wameisifu serikali kwa kuanzisha mfumo wa ukusanyaji mapato kwa njia ya kieletroniki kwa kutumia mashine za "Point of Sale" maarufu kama POS kwani umefanikiwa kuokoa fedha za umma zilizokuwa zinapotelea kwenye mikono ya watu wachache wasio waaminifu.

Akizungumza katika mahojiano maalumu Abdallah Said mkazi wa barabara ya tano jijini Tanga anasema 'Dada nakwambia zamani watu walikuwa wanakula sana kodi zetu, mtu anakupa risiti ya elfu 15 wakati umempa elfu thelathini, lakini baada ya serikali kuleta hizi mashine hakuna wizi kabisa."

Afisa Mapato wa Halmashauri ya Jiji la Tanga, Mustini Mustafa amesema ukusanyaji mapato kwa njia ya POS umekuwa na tija na manufaa kwa Halmashauri kufuatilia mwenendo mzima wa mtu anapokusanya ushuru kutoka katika vyanzo 42 vya mapato katika Halmashauri hiyo.

"Hapo awali kabla ya kuwa na mashine hizi, mtu angeweza kukusanya laki tatu lakini akatengeneza risiti bandia ya laki moja na kupeleka Halmashauri kama makusanyo ya siku hiyo. Ukusanyaji wa mapato kwa njia ya kieletroniki (POS) umesaidia kurahisisha upatikanaji wa taarifa kamili za mapato pamoja na kudhibiti upotevu wa mapato kwa Halmashauri," anafafanua Mustafa.

Sambamba na kusaidia suala la kuokoa fedha, mashine hizo zinazotumika kwenye mfumo wa *"Local Government Revenue Collection Information System-LGRCIS"* zimezidi kuongeza imani kwa wananchi wa Jiji hilo kwani wamekuwa wakiamini pesa hizo zinazokusanywa zinakwenda katika Serikali yao na si kuishia katika mikono ya mafisadi lakini zaidi sana ndizo zinazo saidia masuala ya maendeleo ya nchi.



***Moses Mbwambo Mtendaji wa Mtaa wa Umba jijini Tanga akiwa anatoa risiti kwenye mashine ya POS inliyounganishwa kwenye mfumo wa Makusanyo ya Halmashsuri. (Picha: Tusa Daniel–Tanga Jiji)***

Kwa upande wake Bwana Moses Mbwambo, Mtendaji wa Mtaa wa Umba ndani ya Jiji hilo, yeye hakusita kuonesha furaha yake kwa kuipongeza Serikali kwa hatua hiyo kwani, imewasaidia kuzuia upotevu wa taarifa ambazo awali zilitunzwa kwenye madaftari

Naye Bi. Aisha Abed Msimamizi wa vyoo vya stendi ya Ngamiani amesema kuwa ukusanyaji wa ushuru katika stendi hiyo sasa umeleta tija na chachu kwa wananchi kuamini serikali kwa kuona fedha wanazotoa kupata huduma hiyo zinakwenda moja kwa moja kwenye serikali tofauti na awali ambapo kulikuwa na mianya ya kufujwa.

"Zamani ushuru wa vyoo ndiyo ilikuwa sehemu nzuri ya watu kupiga hela za serikali lakini sasa hivi kila sehemu kumebanwa nakufanya wananchi kuwa na muamko wa kudai risiti pindi wafanyapo malipo" anasema Bi. Aisha

Kitakwimu ukusanyaji wa mapato kwa njia ya kieletroniki katika Jiji la Tanga umeongeza mapato kwa Jiji kutoka Bil10.2 katika mwaka wa fedha 2016/17 hadi Bil.13.1 katika mwaka wa fedha 2018/19 na imeamsha ari na kuibua vyanzo vingi vya mapato kutokana na uaminifu uliopo kupitia mashine hizo, Fedha zinazopatikana zinaelekezwa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo, ilibainika kutoka katika moja ya taarifa kutoka katika Jiji hilo.

***Tusa Daniel– Tanga Jiji***

*KUTOKA DODOMA*

# Halmashauri zapokea Mashine za Kisasa (POS) 7227, Kudhibiti Mianya ya upotevu Mapato

Serikali imezidi kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kukabidhi mashine za (POS) zipatazo 7227 kwa ajili ya kukusanyia mapato kwa njia ya kielektroniki.

Zoezi la kukabidhi mashine za kisasa na zenye utambulisho wa Nembo ya Taifa limefanywa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali Mitaa Mhe. Seleman Jafo (Mb), jijini Dodoma kwa Wakurugenzi wa Halmashauri zote 185.




***Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhandisi Joseph M. Nyamhanga akitoa salaam za Wizara wakati wa zoezi la ugawaji wa mashine za kukusanyia mapato za POS, jijini Dodoma, ambapo katika zoezi hili jumla ya mashine 7227 ziligawanywa kwa Halmashsuri 185 nchini. (Picha: OR-TAMISEMI).***

Akikabidhi mashine hizo Waziri Jafo alisema, kuna watu walikua wanaendelea na ujanja wa kudukua mifumo ya mashine za awali wakati wa kukusanya mapato ikiwemo kubadili tarehe na kuzima mtandao ili fedha hizo zisisomeke kwenye kompyuta kuu *(sever)* lakini sasa suala hilo litafikia ukomo kwa kuanza kutumia mshine mpya.

Mhe. Jafo alisema mashine za awali zilikuwa rahisi katika kubadili baadhi ya taarifa ndiyo maana wameamua kuja na mashine hizo zenye alama za kipekee ambazo zitakabiliana na ukora huo.

"Sasa mwisho wa udanganyifu wa namna hii umekwisha kwani mashine hizi tumeziagiza kutoka kiwandani ambako zimewekewa alama. Vilevile haziruhusu kubadilisha tarehe wala kuzima mtandao hivyo mapato yote yatakayokusanywa kwenye mashine hizi mpya yataonekana kwenye kompyuta kuu (sever) iliyopo makao makuu na kubainika kwa haraka" alisema Mhe. Jafo.

Akizidi kutoa msisitizo, Mhe. Jafo alisema "Tunakwenda kuziba mianya ya wizi ili tuweze kufikia malengo ya ukusanyaji mapato, kwa kuwa katika hili kuna baadhi ya watu wanakatisha tamaa katika suala zima la ukusanyaji mapato kwani hadi mwishoni mwa Desemba, 2019 baadhi ya Halmashauri zilikuwa hazijafikia hata asilimia 20 ya malengo ya makusanyo wakati nyingine zimekusanya zaidi ya asilimia 50," alisisitiza Waziri huyo na kuzitaka Halmashauri hizo kujitathmini.

Akizungumzia kuhusu mashine hizo, alisema zinakwenda kuongeza idadi ya mashine za awali ambazo ni mashine 10,100 kwa Halmashauri zote nchini, hivyo ongezeko hilo litafanya kuwa na jumla ya mashine 17,327 ambazo zitasaidia Halmashauri kuwa na uwezo wa kukusanya mapato zaidi.

Mbali na mashine hizo kutumika katika suala la mapato Mhe. Waziri Jafo alizidi kufafanua kuwa zitatumika kama sehemu ya uzania kwa wakurugenzi kuona kama wanamudu majukumu waliyo kasimiwa, na akaahidi kuwa, ifikapo 30 Aprili, 2020, atatoa tathmini na kisha kumkabidhi Mhe. Rais majina ya wote ambao wataonekana kuwa chini ya viwango walivyojiwekea.

Kwa kuwa suala la ukusanyaji wa mapato imekuwa ni ajenda ya kudumu ya Serikali ya Awamu ya Tano, takwimu zinaonyesha kuwa, Katika kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2015/16 hadi Desemba, 2019/20, Halmashauri, ziliidhinishiwa kukusanya jumla ya shilingi trilioni 2.99. Hadi kufikia Desemba, 2019 mapato halisi ya ndani yalikuwa shilingi trilioni 2.54 sawa na asilimia 85 ya lengo.

Akihutubia mbele ya Wabunge kutoka Kamati ya Bunge juu ya Masuala ya Serikali za Mitaa, Wabunge wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa *LAAC*, Makatibu Tawala wa Mikoa, pamoja na Wakurugenzi walio hudhuria katika hafla hiyo, Waziri alisema wapo baadhi ya Wakurugenzi

***Inaendelea uk. 9***

*Inatoka uk. 8*

## ♦ Mashine za Kisasa Kudhibiti Mianya Upotevu Mapato

wanafanya kazi kwa mazoea, hali inayochangia kwa baadhi ya Halmashauri kushindwa kulipa hata posho za madiwani na akadai kwamba, kuna baadhi ya Halmashauri zinadaiwa na madiwani hadi Shilingi Milioni 758 huku akikabidhi taarifa hiyo ya madai kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais,TAMISEMI, Mhandisi Joseph Nyamuhanga ili aweze kuifanyia kazi.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa OR-TAMISEMI Mhandisi. Joseph Nyamhanga alisema, mashine hizo kila moja ilinunuliwa kwa dola za Merekani zipatazo 140 ambazo ni sawa na shilingi 320,000 wakati bei ya kawaida wangeweza kununua kwa thamani ya shilingi 900,000/= hivyo wameokoa zaidi ya Shilingi, bilioni 4.

Mhandisi Nyamhanga alisema mashine hizo zina Nembo ya Taifa, rangi na haziruhusu kuweka mifumo mingine hata kubadirisha tarehe ambapo amesema njia hiyo ni ya kuwadhibiti wachakachuaji.

"Haya ni mafanikio makubwa kwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuweza kukabidhi mashine hizi ambazo zitasaidia kuongeza mapato ya Halmashauri na kutekeleza miradi ya maendeleo" alihitimisha Katibu Mkuu.

Wakiongea mara baada yakukabidhiwa mashine hizo, Wakurugenzi wa Halmashauri wameipongeza Serikali kwa kuwaongezea mashine za kukusanyia mapato huku wakishauri baadhi ya kasoro ambazo hazijafanyiwa kazi kwenye mfumo wa mapato ziweze kutatuliwa ili mashine hizo mpya zilete tija.

Akiongea kwa niaba ya Wakurugenzi wenzake, Mwenyekiti wa Wakurugenzi Nchini Wakili Kiomoni Kibamba ambaye ni Mkurugenzi wa Jiji la Mwanza alisema, wanaipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano kutokana na jitihada hizo lakini akaiomba OR – TAMISEMI kufanya maboresho ya mfumo wa mapato ili kuongeza ufanisi.




*Katibu Tawala wa Mkoa wa Mkoa wa Lindi Rehema Madenge akikabidhiwa Mashine mpya ya kisasa yakukusanyia mapato ya kieletroniki na Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI, Mhe. Seleman Jafo, ambapo Halmashauri zilikabidhiwa jumla ya mashine 7227 za kisasa. (Picha: OR -TAMISEMI)*

"Kwa sasa mfumo upo kwenye Halmashauri zote, kulikuwa na tatizo la kuzimwa kwa mtandao, hili wamelitibu, unapotumia teknolojia inatakiwa kusiwe na kasoro kwa kiwango cha juu cha madhara kwa maana tekinolojia iweze kutusadia kuzuia wizi kwa asilimia mia moja, pili kulikuwa na fedha zinakusanywa na kutumika kabla ya kupelekwa benki (fedha mbichi) na hivyo kusababisha madeni kwenye mfumo (defaulters). Kwa wanaokusanya mapato wanajua, kwani inabidi kufanya usuluhisho na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa kuangalia mauzo ghafi ya mlipa kodi na ankra ya madai (*bill*) iliyopelekwa na kuangalia kiasi cha fedha kilicholipwa benki taarifa ya benki (*bank statement)* kama fedha zinawiana.

Alisema Kibamba na kuongeza kwamba, "pia wapo mawakala wa kukusanya mapato wasio toa risiti pindi wanapopokea fedha hivyo nimemuomba Mkurugenzi wa TEHAMA, OR - TAMISEMI tuanze kutekeleza mpango wa kulipa kabla ya kukusanya *(float)* na hivyo tutakuwa na suluhu ya kudumu" Alisema Kibamba.

Kabla ya kuanza kutumia mfumo wa kukusanya mapato (LGRCIS) wastani wa makusanyo ukilinganisha na makisio ilikuwa ni asilimia 80 hadi 82 lakini baada yakuanza kutumia mfumo pamoja na jitihada nyingine za Serikali, makusanyo yameendelea kuongezeka nakufikia asilimia 90 ya makisio kwa mwaka wa fedha 2018/19.

***Atley Kuni-TAMISEMI***

### *KUTOKA NJOMBE MJI*

# LGRCIS Yasaidia Halmashauri ya Mji Njombe Kuongeza Bajeti Kufikia Bilioni 4



***Mkusanya ushuru katika stendi ya mabasi Njombe akitoa risiti ya kielekroniki kwa mmoja wa wateja wanaoingia katika stendi hiyo (Picha: Hyasinta Kissima,–Njombe Mji)***

Halmashauri ya Mji Njombe ni miongoni mwa Halmashauri zinazotumia mfumo wa ukusanyaji mapato kwa njia ya Kielektroniki ujulikanao kama LGRCIS. Mfumo wa LGRCIS ulianza kutumika mapema 2016 ambapo kwa kiasi kikubwa umeiwezesha Halmashauri kukusanya mapato yake kikamilifu na hivyo kuifanya kuwa miongoni mwa Halmashauri za Mji zinazoongoza kwenye ukusanyaji wa mapato nchini.

Wakielezea kwa wakati tofauti tofauti watumiaji wa Mfumo wa Ukusanyaji Mapato (LGRCIS) wamesema kuwa licha ya kukusanya mapato lakini pia mfumo umewezesha kukabiliana na vyanzo vya upotevu wa mapato, uvamizi wakati wa kukusanya mapato na hivyo kuiwezesha Halmashauri kuongeza makisio ya ukusanyaji wa mapato kutoka Bilioni 3.09 kwa mwaka wa fedha 2019/20 mpaka kufikia bilioni 4.1 kwa mwaka 2020/21 kwani mteja au mkusanya ushuru pindi anapotengenezewa bili inamlazimu kulipa kwa wakati.

“Tunafanya vikao vya Menejimenti kila Jumatatu agenda kuu ni ukusanyaji mapato. Taarifa za mapato zinazotolewa kwenye Mfumo wa LGRCIS huwa zinajadiliwa katika kila chanzo, kila geti na vituo vya kukusanyia ushuru. Kwa juma zima tunajua tumekusanya kiasi cha shilingi ngapi na endapo makusanyo yasipofikia kiasi tulichokisia, lazima tuulizane na tupate suluhu ya sababu iliyosababisha upungufu wa mapato katika wiki husika. Mfumo ndio unatuwezesha kupata taarifa sahihi ya nini kinaenda kujadiliwa, isingekuwa mfumo ingekuwa ngumu kujua tumekusanya nini. Hii ndio siri ya sisi kukusanya zaidi na mpaka sasa katika mwaka wa fedha ujao tuna mapendekezo ya kuongeza bajeti yetu,” anasema George Mwaseba Mhasibu wa Mapato Halmashauri ya Mji Njombe.

Mwaseba anaendelea kusema kuwa matumizi ya mfumo wa LGRCIS yamesaidia kwa kiasi kikubwa Halmashauri kuweza kujitegemea na kufanikiwa kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa miundombinu katika sekta ya afya na elimu, kutokana na ukusanyaji mzuri wa mapato imesaidia kujenga imani kubwa kwa wananchi kwani pindi malipo yanapofanyika risiti za kielektroniki hutolewa na hivyo kufanya wananchi kuwa na muamko wakulipa mapato ya Halmashauri

“Kabla ya

***Inaendelea uk. 11***

*Inatoka uk. 10*

## ♦ *LGRCIS Yasaidia Halmashauri ya Mji Njombe*

mfumo iliwalazimu wananchi kutumia muda mwingi kuja Halmashauri kulipa bili. Kwa sasa mfumo umeokoa muda na kuepusha usumbufu. Unaweza kumtumia namba ya malipo na baadae akalipa kupitia mawakala waliopo katika maeneo ya Miji au Vijijini," anaeleza Mwaseba

Mwaseba anaongeza kuwa licha ya kuokoa muda pia imeipunguzia Halmashauri gharama za ununuzi wa vitabu, matumizi ya mafuta na magari kwa ajili ya kukusanya mapato ambapo kwa sasa kupitia mfumo wa mapato wakusanya ushuru wanaweza kuhifadhi mapato yaliyokusanywa kupitia mawakala walio karibu na maeneo yao ya kazi.

Kwa upande wao Edward Mhina na Upendo Mwankemwa kutoka Kitengo cha Biashara wanasema kuwa matumizi ya mfumo wa mapato yamesaidia katika kurahisisha utendaji kazi kwani mteja anapofanya malipo mfumo unakuongoza kuchagua kifungu cha malipo husika na mapato hupelekwa kwenye kifungu husika jambo ambalo limewarahisishia kutoa huduma kwa muda mfupi na hivyo kuweza kuhudumia watu wengi zaidi.

Aidha, kupitia mfumo wa LGRCIS imewawezesha kuwa na taarifa sahihi za wafanyabiashara na kurahisisha ufuatiliaji wa mapato.

Baadhi ya wanufaika wa matumizi ya LGRCIS akiwemo Salome Mbilinyi ambaye ni mfanyabiashara wa vinywaji na Jeminy Mbwilo mfanyabiashara wa mbao wanasema kuwa, matumizi ya mfumo yameokoa muda wao mwingi kwani kwa sasa wanaweza kulipia leseni za biashara zao kupitia Wakala wakiwa katika maeneo yao ya biashara. Vilevile wameelezea kuwa, matumizi ya risiti za kielektroniki yamewajengea imani ya kuendelea kulipa ushuru kwani wanaamini kuwa ushuru wanaolipa unakwenda kusaidia shughuli za maendeleo katika Halmashauri yao ambapo awali matumizi ya vitabu yalififisha imani ya ulipaji mapato.

Licha ya kuwa na changamoto kadha wa kadha katika Mfumo wa LGRCIS lakini Halmashauri inaona suala la uwepo wa mashine ni ukombozi. Mfumo wa ukusanyaji Mapato ni moja kati ya jitihada kubwa iliyofanywa na Serikali katika kuhakikisha kuwa Halmashauri zinajiendesha kupitia makusanyo yake na matumizi ya mashine za kukusanyia mapato Point of Sales (POS) yamesaidia kudhibiti upotevu wa mapato na hivyo kuiwezesha Halmashauri kukusanya zaida.




***Mkusanya ushuru katika stendi ya mabasi Njombe akitoa risiti ya kielekroniki kwa dereva wa basi linalofanya safari zake ndani ya Mkoa wa Njombe (Picha: Hyasinta Kissima,–Njombe Mji)***

***Hyasinta Kissima,–Njombe Mji***

*KUTOKA KONDOA MJI*

# LGRCIS Mkombozi wa Makusanyo ya Mapato Kondoa

LGRCIS ni miongoni mwa mifumo inayotumika kuvuna taarifa sahihi za ukusanyaji mapato kwa muda wowote.

Katika hatua nyingine, uwepo wa mashine ya POS imechangia mazingira wezeshi kurahisisha ukusanyaji wa mapato katika vituo mbalimbali. Mashine hizi hutumia mtandao na zimeunganishwa kuweza kuwasiliana na mfumo mkuu wa LGRCIS.

Halmashauri ya Mji Kondoa ni miongoni mwa Halmashauri zinazotumia mfumo huu ambapo ilianza kutumia mwaka 2016 na kwa kiasi kikubwa umekuwa ni msaada mkubwa kwa kuongeza asilimia ya makusanyo na kuongeza imani kwa wananchi wanaopatiwa risiti baada ya kulipia huduma mbalilmbali.

Afisa Mapato wa Halmashauri ya Mji Kondoa Jonathan Gertad alisema kuwa mfumo huo kwake umemsaidia kupunguza majadiliano na mteja kwa kuwa viwango vilivyowekwa ndivyo vinavyotoka na mkusanya ushuru hawezi kubadilisha viwango bila kuwasiliana naye kwa kuandika barua ya sababu ya kupunguza viwango hivyo na imenisaidia kupata mapato halisi ambayo yamewekwa kwenye bajeti.

"Lakini pia mfumo huu umepunguza gharama za kwenda kufuatilia mapato katika maeneo mbalimbali ambapo ilinilazimu kuongozana na mtunza fedha, dereva na mimi ili kuhakikisha fedha zinakusanywa na katika gari uweke mafuta lakini kwasasa naweza kufuatilia fedha hizo nikiwa ofisini na kujua kila mtu kakusanya kiasi gani kila sekunde kwa kuangalia ukurasa wa Mfumo wa Mapato (LGRCIS Dashboard)," amesema Gertad.



*Afisa Mifugo na Uvuvi Halmashauri ya Mji Kondoa Bi. Monica Kimario (wa kwanza kushoto) akitoa risiti kwa kutumia POS kwa wafugaji wakati wa zoezi la utoaji wa chanjo ya kimeta katika kata ya Kingale. (Picha: Stella Kalinga-Kondoa Mji)*

Ameongeza kuwa usalama wa fedha umeongezeka kwakutumia mashine, kwakuwa awali ilikuwa vigumu kutambua kutokana na kutumia vitabu, kiasi kilichokusanywa kiliwafanya wakusanya mapato wengi kutupa vitabu au kuvificha ukienda kufuatilia mapato na kwa kuwa hujui kiasi kamili kilichokusanywa unapewa fedha kidogo ambapo kwasasa ni rahisi kujua unapoona mkusanyaji haweki fedha benki unamfuatilia ukijua kiasi kamili alichokusanya.

Bwana Issa Hussen Kiberenge ni mmoja wa wakusanya mapato katika stendi ya mabasi ya Kondoa Mjini ambapo magari yote yanayoingia ndani ya stendi yanapaswa kulipiwa ushuru na mkusanyaji ameunganishwa katika mfumo wa kielektroniki kwa kutumia mashine ya POS na wateja wote wanapewa risiti za kielektroniki za mfumo tofauti na zamani ambapo walikuwa wakitumia risiti za kuandika kwa mkono na ametoa maoni yake kuhusu mfumo huo kwa upande wake.

***Inaendelea uk. 13***

*Inatoka uk. 12*

## ♦ *LGRCIS Mkombozi wa Makusanyo ya Mapato Kondoa*




*Bwana Issa Hussein Kiberenge akiwakatia risiti katika POS wateja wanaotoka katika stendi ya Mabasi Kondoa Mjini. (Picha: Stella Kalinga-Kondoa Mji)*

"Matumizi ya POS yamenisaidia sana katika kazi yangu maana najua kiasi nilichokusanya kwa siku husika ninapoitoa tu taarifa ya siku husika, lakini pia unanisaidia aina za magari nilizokatia ushuru katika siku husika inakuwa kama ni sensa pia kwa sehemu yangu ya kukusanya ushuru ambapo zamani ilikuwa hadi nianze kupitia vitabu na kuhesabu ambapo ilikuwa inachukua muda mwingi."

Ameongeza kuwa utumiaji wa mfumo ulikuja sambamba na uwekaji wa mageti katika stendi na uzibaji wa vichochoro ambapo kwasasa ameongeza ukusanyaji wa mapato ambapo awali alikuwa akikusanya shilingi laki tano 500,000 kwa wiki na sasa anakusanya shilingi laki nane 800,000 kwa wiki hivyo umemwongezea uwajibikaji.

Mtendaji wa Mtaa wa Mnarani Idafrosa Ambrose ambaye pia katika shughuli za kukusanya fedha katika Mtaa wake anatumia mashine za kukusanyia mapato amesema kuwa kutumia mfumo huo kumefanya uaminifu uongezeke kwa wananchi wa Mtaa wake ambao kwasasa bila kupatiwa risiti za mfumo hawakubali kutoa fedha za mchango wowote.

"Unajua zamani tulikuwa tunatumia madaftari kukusanyia fedha hasa za usafi unaenda kwa mwananchi unamuandika jina kwenye daftari anakupa fedha lakini kwasasa toka tuanze kutumia mashine za kielektroniki kukusanyia mapato mwananchi hakubali kuandikwa jina kwenye daftari anataka risiti ya mfumo tu na ukimpa wala halalamiki kwa kweli wameturahisishia sana kazi," amesema Ambrose.

Aidha ameongeza kuwa pamoja na faida za mfumo pia kuna changamoto ndogondogo ambazo hutatuliwa kwa muda mfupi hasa kukatika kwa mtandao unapokuwa na mteja ambapo wenye haraka huondoka na fedha hadi mtandao unaporudi japokuwa ni mara chache sana matatizo hayo hutokea.

Ambrose ameongeza kuwa matumizi ya mashine ya POS yamesaidia sana kunipa amani ya kazi sababu mapato mengi yanatokana na fedha za uzoaji taka tunafanya kazi na kamati na ndio mhusika na fedha zote zinaingia kwenye mfumo ile migogoro ya kulaumiana kutoa fedha nje ya mfumo hayapo maana hadi iingizwe benki naomba tu mfumo uendelee niendelee kufanya kazi kwa amani.

"Kwasasa nina kitabu nimechukua kwa ajili ya kukusanya fedha za sungusungu wa usiku na ujenzi wa Ofisi ya Mtaa lakini wananchi hawana imani na risiti hizi na kiutaratibu fedha hizi hutumii mashine za ukusanyaji mapato hivyo inanipa wakati mgumu kumuelewesha mwananchi ila ingekuwa risiti ya kielektroniki hawana shida wanajua fedha inaenda moja kwa moja serikalini," amesisitiza Ambrose.

***Stella Kalinga -KONDOA***